# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

***(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)***

**Sehemu ya CXXXIV Nam. 7311** **10 Febuari , 2025** **Bei Shs. 4,000/=**
*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* *Hutolewa kila Ijumaa*

**YALIYOMO** *Ukurasa*

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu, Nam. 2 ya 2012 na Kutunga Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Kisiasa kwa ajili ya Kuweka Masharti ya Kutoa Mafao na Huduma kwa Viongozi Waliostaafu Utumishi wa Kisiasa na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo ............................ 225

## SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Mswada lililotajwa hapo chini linatangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

### Tangazo la Mswada

Nam. :- Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu, Nam. 2 ya 2012 na Kutunga Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Kisiasa kwa Ajili ya Kuweka Masharti ya Kutoa Mafao na Huduma kwa Viongozi Waliostaafu Utumishi wa Kisiasa na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo

### TANGAZO

Mswada ufuatao utawasilishwa katika Mkutano wa Baraza la Wawakilishi utakaoanza tarehe 12 Febuari, 2025 kwa kusomwa mara ya kwanza, ya pili na ya tatu na unachapishwa pamoja na Madhumuni na Sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa wananchi.

**ZANZIBAR** (Mhandisi Zena Ahmed Said)
10 Febuari, 2025 ***Katibu wa Baraza la Mapinduzi***
***na Katibu Mkuu Kiongozi.***

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

**MSWADA**
***wa***
**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA MAFAO YA VIONGOZI WA KISIASA WASTAAFU, NAM. 2 YA 2012 NA KUTUNGA SHERIA YA MAFAO YA KUSTAAFU UTUMISHI WA KISIASA KWA AJILI YA KUWEKA MASHARTI YA KUTOA MAFAO NA HUDUMA KWA VIONGOZI WALIOSTAAFU UTUMISHI WA KISIASA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1**. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Kisiasa, 2025 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais.

Ufafanuzi.

**2**. Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"asilimia maalumu" maana yake ni asilimia maalumu inayoamuliwa na Rais kwa ajili ya utoaji wa kiinuwa mgongo na posho la hitimisho la kazi;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Zanzibar ya 1984;

"kiinua mgongo" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa mkupuo kwa kiongozi wa kisiasa baada ya kusita au kumaliza muda wa kushika nafasi hiyo;

"kiongozi wa kisiasa" maana yake ni mtu anayetumikia au aliyetumikia nafasi ya Rais, Makamo wa Rais, Mwanasheria Mkuu, Waziri, Naibu Waziri, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi;

"mafao" maana yake ni pencheni, kiinua mgongo, posho la hitimisho la kazi au stahiki nyengine yoyote inayotolewa chini ya msharti ya Sheria hii;

"Makamo wa Rais" maana yake ni Makamo wa Kwanza wa Rais na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar;

"mamlaka husika" maana yake ni, kuhusiana na utoaji wa mafao kwa:

(a) Rais Mstaafu na Makamo wa Rais Mstaafu maana yake Katibu Mkuu anayehusika na mambo ya Rais;

(b) Mwanasheria Mkuu Mstaafu, Waziri Mstaafu na Naibu Waziri Mstaafu maana yake ni Katibu Mkuu anayehusika na Utumishi wa Umma; na

(c) Spika Mstaafu, Naibu Spika Mstaafu na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi maana yake ni Katibu wa Baraza la Wawakilishi;

"mamlaka ya uteuzi" maana yake ni Rais, Tume ya Uchaguzi au Baraza la Wawakilishi;

"mjane wa kike au mjane wa kiume" maana yake ni aliyekuwa mke au mume wa Rais, Makamo wa Rais au Spika aliyefariki akiwa madarakani au baada ya kusita au kumaliza muda wa kushika nafasi hiyo;

"mshahara" maana yake ni mshahara halisi wa kiongozi wa kisiasa usiyojumuisha posho la aina yoyote;

"mtegemezi" kuhusiana na Kiongozi wa Kisiasa aliyefariki maana yake ni:

(a) endapo kiongozi wa kisiasa aliyefariki alikuwa mwanamme, mjane au wajane wake, baba, mama, mtoto au watoto; au

(b) endapo kiongozi wa kisiasa aliyefariki ni mwanamke, mjane wake, baba, mama, mtoto au watoto;

"mtumishi wa umma" maana yake ni muajiriwa katika utumishi wa umma;

"posho" maana yake ni stahiki zozote zisizokuwa mshahara;

"Rais Mstaafu" maana yake ni mtu aliyeshika nafasi ya Rais wa Zanzibar, lakini amesita au amemaliza muda wa kushika nafasi hiyo na maneno "Makamo wa Rais Mstaafu", "Waziri Mstaafu" na "Naibu Waziri Mstaafu" yatatafsiriwa ipasavyo;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Spika Mstaafu" maana yake ni mtu aliyeshika nafasi ya Spika wa Baraza la Wawakilishi lakini amesita au amemaliza muda wa kushika nafasi hiyo na maneno "Naibu Spika Mstaafu na "Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wastaafu" yatatafsiriwa ipasavyo;

"utumishi wa kisiasa" maana yake ni utumishi katika nafasi ya Rais, Makamo wa Rais, Mwanasheria Mkuu, Waziri, Naibu Waziri, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi;

"utumishi wa umma" maana yake ni utumishi wowote chini ya usimamizi wa moja kwa moja wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ au Tume ya utumishi nyengine yoyote na itajumuisha utumishi katika wakala na taasisi za umma na

endapo mazingira yatahitaji pia itajumuisha utumishi katika mashirika ya umma ambapo hisa kubwa zinamilikiwa na Serikali; na

"Waziri anayehusika" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala yanayohusiana na mambo ya Rais.

## SEHEMU YA PILI
## MASHARTI YANAYOSIMAMIA UTOAJI WA MAFAO

Mawanda ya kustahiki kupatiwa mafao.

**3**.-(1) Kiongozi wa kisiasa atastahiki kupewa mafao chini ya Sheria hii ikitokea moja kati ya yafutayo:

(a) amemaliza kipindi cha utumishi katika nafasi ambayo amechaguliwa au kuteuliwa;

(b) ameacha kutumikia nafasi yake ya utumishi kwa mujibu wa masharti ya Katiba au sheria nyengine yoyote inayotumika Zanzibar;

(c) kufutwa kwa ofisi ambayo amechaguliwa au kuteuliwa;

(d) kuwepo kwa ushahidi wa kitabibu unaothibitisha kwamba hana uwezo wa kutekelza majukumu yake katika nafasi hiyo aliyochaguliwa au kuteuliwa;

(e) amefariki akiwa kiongozi wa kisiasa kabla ya kumaliza muda wake wa utumishi ambapo mafao watapewa wategemezi wake;

(f) kusitishwa kwa uteuzi wake katika nafasi hiyo na mamlaka ya uteuzi;

(g) kuteuliwa katika nafasi nyengine ambayo atalazimika kuacha nafasi ya kisiasa kwa mujibu wa sheria.

(2) Endapo mtu kabla ya kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Rais, Makamo wa Rais au Spika alikuwa ameajiriwa kwa mujibu wa masharti ya pencheni au ajira yake inasimamiwa na mfuko wa mafao ya kumaliza utumishi ambapo mafao ya kustaafu kazi au kutoka katika mfuko wa mafao yalikuwa katika namna ya malipo ya pencheni, haki ya mtu huyo ya kupokea mafao ya pencheni ya kumaliza utumishi chini ya mfuko huo yatasita na atastahiki kupewa mafao chini ya Sheria hii.

Kutokuwa na sifa ya kustahiki mafao.

**4**. Kiongozi wa kisiasa hatostahiki mafao chini ya Sheria hii ikiwa ataacha nafasi yake ya kisiasa katika hali iliyothibitishwa amekosa uaminifu na heshima kwa Zanzibar chini ya Katiba au sheria nyengine yoyote.

Taratibu za kuondo-lewa sifa za kustahiki kulipwa mafao.

**5**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria hii, Rais atamteua Mwenyekiti na wajumbe wengine wawili ambao ni Majaji au wenye sifa za kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar ili kuchunguza tuhuma ambazo zitathibitisha kutokustahiki kupewa mafao chini ya Sheria hii.

(2) Taratibu za kufanya uchunguzi na mambo yanayohusiana na hayo chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki zitaelezwa katika kanuni.

Upokeaji wa mafao ya kumaliza utumishi kutoka mifuko mengine.

**6**.- (1) Endapo kiongozi wa kisiasa isipokuwa Rais Mstaafu, Makamo wa Rais Mstaafu au Spika Mstaafu kabla ya kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa kiongozi wa kisiasa, alikuwa mtumishi wa umma aliyeajiriwa kwa mujibu wa masharti ya pencheni au ajira yake ilikuwa ikisimamiwa na mfuko wa mafao ya kumaliza utumishi ambapo mafao ya kumaliza utumishi yalikuwa katika namna ya malipo ya pencheni, kipindi ambacho alitumikia kama kiongozi wa kisiasa kitachukuliwa kwa madhumuni ya kuhesabu pencheni au kiinua mgongo iwapo kiongozi huyo wa kisiasa amechangia kwa hiari na anaweza kupewa chini ya sheria za pencheni zinazosimamia ajira yake kama mtumishi wa umma.

(2) Endapo kiongozi wa kisiasa, isipokuwa Rais Mstaafu, Makamo wa Rais Mstaafu au Spika Mstaafu ambaye kabla ya kuwa kiongozi wa kisiasa alikuwa mtumishi wa umma na ambaye, baada ya kusita kuwa kiongozi wa kisiasa hajafikia umri wa kustaafu, pencheni au kiinua mgongo chake kitahesabiwa kwa mujibu wa masharti ya sheria ambayo ilikua inasimamia ajira yake kama mtumishi wa umma kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Mafao kulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

**7.** Mafao yote chini ya Sheria hii yatalipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

Msahama wa kodi ya mapato.

**8**. Mafao yote yanayotolewa kwa kiongozi wa kisiasa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii yatasamehewa kodi ya mapato.

## SEHEMU YA TATU
## UTOAJI WA MAFAO KWA RAIS MSTAAFU, MAKAMU WA RAIS MSTAAFU, SPIKA MSTAAFU NA NAIBU SPIKA MSTAAFU

Mafao kwa Rais Mstaafu.

**9**.-(1) Mtu ambaye alishika nafasi ya Rais wa Zanzibar, baada ya kusita au kumaliza muda wa kushika nafasi hiyo, atapewa mafao kama yalivyoainshwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

(2) Rais anaweza kuchukua hatua nyengine zozote zinazofaa kwa ajili ya kulinda hadhi na heshima ya Rais Mstaafu.

Kiinua mgongo kwa wategemezi wa Rais aliyefariki.

**10**. Endapo Rais atafariki akiwa madarakani au atafariki baada ya kustaafu na ikawa hakuwahi kulipwa mafao yake, Mamlaka inayohusika itatoa kiinua mgongo kwa wategemezi wake ambacho kitakuwa sawa na kiinua mgongo alichostahiki kupokea kama angelikuwa hai.

Mafao kwa Makamo wa Rais Mstaafu.

**11**.-(1) Mtu ambaye alishika nafasi ya Makamo wa Rais wa Zanzibar, baada ya kusita au kumaliza muda wa kushika nafasi hiyo, atapewa mafao kama yalivyoaninshwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

(2) Kwa madhumuni ya masharti ya Sheria hii, Waziri Kiongozi Mstaafu wa Zanzibar atachukuliwa kama ni Makamo wa Pili wa Rais Mstaafu wa Zanzibar.

Kiinua mgongo kwa watege-mezi wa Makamo wa Rais aliyefariki.

**12**. Endapo Makamo wa Rais atafariki akiwa madarakani au atafariki baada ya kustaafu na ikawa hakuwahi kulipwa mafao yake, Mamlaka inayohusika itatoa kiinua mgongo kwa wategemezi wake ambacho kitakuwa sawa na kiinua mgongo alichostahiki kupokea kama angelikuwa hai.

Mafao kwa Spika Mstaafu.

**13**. Mtu ambaye alishika nafasi ya Spika wa Baraza la Wawakilishi, baada ya kusita au kumaliza muda wa kushika nafasi hiyo, atapewa mafao kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

Kiinua mgongo kwa watege-mezi wa Spika aliyefariki.

**14**. Endapo Spika atafariki akiwa madarakani au atafariki baada ya kustaafu na ikawa hakuwahi kulipwa mafao yake, Mamlaka inayohusika itatoa kiinua mgongo kwa wategemezi wake ambacho kitakuwa sawa na kiinua mgongo alichostahiki kupokea kama angelikuwa hai.

Mafao kwa Naibu Spika Mstaafu.

**15**. Mtu ambaye alishika nafasi ya Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, baada ya kusita au kumaliza muda wa kushika nafasi hiyo, atapewa mafao kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii.

Kiinua mgongo kwa watege-mezi wa Naibu Spika aliyefariki.

**16**. Endapo Naibu Spika atafariki akiwa madarakani au atafariki baada ya kustaafu na ikawa hakuwahi kulipwa mafao yake, Mamlaka inayohusika itatoa kiinua mgongo kwa wategemezi wake ambacho kitakuwa sawa na kiinua mgongo alichostahiki kupokea kama angelikuwa hai.

Kusitishwa kwa baadhi ya mafao.

**17**.-(1) Bila ya kujali masharti ya Sheria hii, Rais Mstaafu, Makamo wa Rais Mstaafu au Spika Mstaafu hatopewa mafao yaliyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii isipokuwa kiinua mgongo na posho la hitimisho la kazi ikiwa ataacha ofisi moja ya kisiasa na kuingia ofisi nyengine ya kisiasa iliyotangazwa na Sheria hii kama ofisi maalumu ya kitaifa isipokuwa atakapoacha au kustaafu kutoka ofisi hiyo maalumu ya kitaifa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, neno “ofisi maalumu ya kitaifa” maana yake Ofisi ya Rais wa Zanzibar, Ofisi ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Makamo wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Makamo wa Rais wa Zanzibar, Ofisi ya Spika wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Spika wa Baraza la Wawakilishi.

Matunzo ya mtoto au watoto wa kiongozi wa Rais, Makamo wa Rais na Spika aliyefariki akiwa madara-kani.

**18**. Endapo Rais, Makamo wa Rais au Spika wa Baraza la Wawakilishi atafariki akiwa madarakani, mtoto au watoto wake walio chini ya miaka kumi na nane watatunzwa na mamlaka husika mpaka mtoto au watoto hao watakapofikia umri wa miaka ishirini na tano au atakapopata kazi itakayompatia mshahara, au chochote kitakachokuja mwanzo.

## SEHEMU YA NNE
## UTOAJI WA MAFAO KWA MWANASHERIA MKUU MSTAAFU, WAZIRI MSTAAFU, NAIBU WAZIRI MSTAAFU NA MJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI MSTAAFU

Mafao kwa Mwana-sheria Mkuu, Waziri, Naibu Waziri, na Mjumbe wa Baraza la Wawaki-lishi Mstaafu.

**19**.-(1) Waziri, Mwanasheria Mkuu, Naibu Waziri na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, baada ya kumaliza muda wa utumishi, atapewa kiinua mgongo na posho la hitimisho la kazi kama iliyoelezwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii.

(2) Malipo ya kiinua mgongo yaliyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki yatahesabiwa kulingana na idadi ya miezi ambayo Waziri, Mwanasheria Mkuu, Naibu Waziri na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ameshika nafasi hiyo.

(3) Posho la hitimisho la kazi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki litalipwa baada ya kumaliza utumishi na litahesabiwa kwa kuzingatia kila mwaka wa utumishi uliokamilika kama ilivyoainishwa chini ya Jadweli la Pili la Sheria hii.

(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki "kila mwaka wa utumishi uliokamilika" maana yake ni miezi kumi na mbili au sehemu yoyote ya mwaka husika.

(5) Waziri mstaafu, Naibu Waziri Mstaafu na Mwanasheria Mkuu mstaafu atapatiwa mafao mengine kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Pili la Sheria hii.

(6) Kwa madhumuni ya utoaji wa mafao chini ya kifungu hiki, endapo Rais atavunja Baraza la Wawakilishi kabla ya kufikia muda wa uhai wake kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika Katiba, itahesabika kuwa Baraza limemaliza muda wa uhai wake.

Kiinua mgongo kwa wategemezi wa Waziri, Mwana-sheria Mkuu, Naibu Waziri, na Mjumbe wa Baraza la Wawaki-lishi aliyefariki.

**20**. Endapo Waziri, Mwanasheria Mkuu, Naibu Waziri au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi atafariki akiwa madarakani au atafariki baada ya kustaafu na ikawa hakuwahi kulipwa mafao yake, Mamlaka inayohusika itatoa kiinua mgongo kwa wategemezi wake ambacho kitakuwa sawa na kiinua mgongo alichostahiki kupokea kama angelikuwa hai.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI MENGINEYO

Kuzuiliwa kulipwa mafao.

**21**. Bila ya kujali masharti ya kifungu cha 3(1)(f) na kifungu cha 19(1) cha Sheria hii, endapo Makamo wa Pili wa Rais, Waziri na Naibu Waziri amesita katika nafasi yake kabla ya kumaliza muda wake au kuvunjwa kwa Baraza la Wawakilishi lakini anaendelea kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, hatostahiki mafao yake mpaka atakaposita kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na mafao yake yatazingatia mishahara yote aliyopokea wakati wa muda wa kuwa kiongozi wa kisiasa.

Mafao kwa mwenza, mjane wa kike au mjane wa kiume wa Rais Mstaafu, wa Makamo wa Rais Mstaafu na wa Spika Mstaafu.

**22**. Mwenza, mjane wa kike au mjane wa kiume wa Rais Mstaafu, Makamo wa Rais Mstaafu na Spika Mstaafu watapewa mafao kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Tatu la Sheria hii.

Muda wa malipo ya kiinua mgongo na posho la hitimisho la kazi.

**23**. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, kiongozi wa kisiasa atastahiki kulipwa kiinua mgongo na posho la hitimisho la kazi ndani ya miezi mitatu baada ya kusita au kumaliza utumishi katika nafasi ya kisiasa.

Ugawaji wa kiinua mgongo kwa wategemezi.

**24**. Ugawaji wa kiinua mgongo kwa wategemezi chini ya Sheria hii, utakuwa kwa mujibu wa Sheria ya mirathi ambayo kiongozi wa kisiasa aliyefariki anahusika.

Marekebisho ya Jadweli.

**25**. Waziri anayehusika anaweza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, kwa kushauriana na Katibu Mkuu Kiongozi na baada ya kuidhinishwa na Rais, kurekebisha jadweli lolote la Sheria hii.

Uwezo wa Rais kutoa mafao mengine.

**26**. Bila ya kuathiri masharti ya Sheria hii, Rais anaweza, atakapoona inafaa kutoa mafao ya ziada chini ya Sheria hii.

Kanuni.

**27**. Waziri anayehusika anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Kufuta na kubakiza.

**28**.-(1) Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu, Nam. 2 ya 2012 inafutwa.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mafao yoyote yaliyotolewa chini ya Sheria iliyofutwa yatachukuliwa kama yametolewa chini ya masharti ya Sheria hii.

## JADWELI LA KWANZA

## MAFAO KWA RAIS MSTAAFU, MAKAMO WA RAIS MSTAAFU, SPIKA MSTAAFU NA NAIBU SPIKA MSTAAFU

**[Chini ya kifungu cha 9, 11, 13 na 15]**

---

### A: MAELEZO YA MAFAO ANAYOPEWA RAIS MSTAAFU

**1.** Kiinua mgongo sawa na asilimia hamsini ya mshahara mkubwa aliowahi kupokea ukizidishwa na idadi ya miezi aliyoshika nafasi hiyo kama Rais.

**2**. Posho la hitimisho la kazi sawa na kiwango ambacho alipokea kama mshahara mkubwa ukizidishwa na miezi ishirini na nne.

**3**. Pencheni inayotolewa kila mwezi sawa na asilimia themanini ya mshahara wa Rais aliyopo madarakani.

**4**. Umiliki wa nyumba yenye samani na vyumba visivyopungua vinne vya kulala ambapo angalau vyumba viwili vitakuwa vinajitegemea, na itakayokuwa na ofisi yenye samani na sehemu ya kukaa mtumishi.

**5**. Posho la matunzo la kila mwezi sawa na asilimia themanini ya posho la matunzo analolipwa Rais aliyopo madarakani.

**6**. Huduma za matibabu ndani na nje ya Zanzibar zitakazolipwa na Serikali.

**7**. Huduma za Maji na umeme zitakazolipwa na Serikali.

**8**. Watumishi saba na walinzi wawili.

**9**. Posho la simu kwa kila mwezi kwa kiwango cha Shilingi laki nane.

**10**. Gari tatu zitakazotolewa na Serikali na kubadilishwa kila baada ya miaka mitano, na dereva watatu.

**11**. Posho la mafuta, matunzo na gharama za kuendeshea gari hizo kama itakavyotolewa kwa Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kila gari.

**12**. Ulinzi na huduma nyengine za ulinzi.

**13**. Hati za kusafiria zenye hadhi ya kidiplomasia na matumizi ya kumbi za wageni mashuhuri kwa ajili yake, mwenza, baba, mama na watoto wake walio chini ya umri wa miaka kumi na nane.

**14**. Malipo ya gharama za safari daraja la kwanza ambazo zitahusisha mwenza wake na wasaidizi wawili binafsi wakati atakapotakiwa kusafiri na Serikali au taasisi za kimataifa ndani na nje ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na ikitokea kusafiri ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania gharama pia zitahusisha dereva au ikiwa ni kusafiri kimatibabu pia zitahusisha daktari binafsi.

**15**. Malipo ya gharama za safari binafsi daraja la kwanza zisizozidi nne kwa mwaka ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na moja kwa mwaka nje ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zitahusisha mwenza, baba, mama, watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na nane wasiozidi wawili na wasaidizi wawili, na ikiwa safari ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania gharama pia zitahusisha dereva; ambapo safari hiyo haitozidi siku kumi.

**16**. Watumishi wa ndani na walinzi wa ziada atapatiwa pindi itakapohitajika.

**B: MAELEZO YA MAFAO ANAYOPEWA MAKAMO WA RAIS MSTAAFU**

**1**. Kiinua mgongo sawa na asilimia hamsini ya mshahara mkubwa aliowahi kupokea ukizidishwa na idadi ya miezi aliyoshika nafasi hiyo kama Makamo wa Rais.

**2**. Posho la hitimisho la kazi sawa na kiwango ambacho alipokea kama mshahara mkubwa ukizidishwa na miezi ishirini na nne.

**3**. Pencheni inayotolewa kila mwezi sawa na asilimia themanini ya mshahara wa Makamo wa Rais aliyopo madarakani.

**4**. Makaazi au asilimia hamsini ya pencheni ya kila mwezi au Shilingi Milioni Tano au chochote kitakachokua kikubwa kati ya hivyo, itakayolipwa kama posho la nyumba kwa mwezi.

**5**. Posho la matunzo la kila mwezi sawa na asilimia themanini ya posho la matunzo analolipwa Makamo wa Rais aliyopo madarakani.

**6**. Huduma za matibabu ndani na nje ya Zanzibar zitakazolipwa na Serikali.

**7**. Huduma za Maji na umeme zitakazolipwa na Serikali.

**8**. Watumishi watano na walinzi wawili.

**9**. Posho la simu kwa kila mwezi kwa kiwango cha Shilingi laki sita.

**10**. Gari mbili zitakazotolewa na Serikali na kubadilishwa kila baada ya miaka mitano, na dereva wawili.

**11**. Posho la mafuta, matunzo na gharama za kuendeshea gari hizo kama itakavyotolewa kwa Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kila gari.

**12**. Ulinzi na huduma nyengine za ulinzi.

**13**. Hati za kusafiria zenye hadhi ya kidiplomasia na matumizi ya kumbi za watu mashuhuri kwa ajili yake, mwenza, baba, mama na watoto wake walio chini ya umri wa miaka kumi na nane.

**14**. Malipo ya gharama za safari daraja la kwanza ambazo zitahusisha mwenza wake na msaidizi mmoja binafsi wakati atakapotakiwa kusafiri na Serikali au taasisi za kimataifa ndani na nje ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na ikitokea kusafiri ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania gharama pia zitahusisha dereva au ikiwa ni kusafiri kimatibabu pia zitahusisha daktari binafsi.

**15.** Malipo ya gharama za safari binafsi daraja la kwanza zisizozidi tatu kwa mwaka ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na moja kwa mwaka nje ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zitahusisha mwenza, baba, mama, watoto walio chini ya umri wa miaka kumi na nane wasiozidi wawili na msaidizi mmoja, na ikiwa safari ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania gharama pia zitahusisha dereva; ambapo safari hiyo haitozidi siku kumi.

**16**. Watumishi wa ndani na walinzi wa ziada atapatiwa pindi itakapohitajika.

**C: MAELEZO YA MAFAO ANAYOPEWA SPIKA MSTAAFU**

**1**. Kiinua mgongo sawa na asilimia hamsini ya mshahara mkubwa aliowahi kupokea ukizidishwa na idadi ya miezi aliyoshika nafasi hiyo kama Spika.

**2**. Posho la hitimisho la kazi sawa na kiwango alichopokea kama mshahara mkubwa ukizidishwa na miezi ishirini na nne.

**3**. Pencheni inayotolewa kila mwezi sawa na asilimia themanini ya mshahara wa Spika aliyopo madarakani.

**4**. Makaazi au asilimia hamsini ya pencheni ya kila mwezi itakayolipwa kama posho la nyumba.

**5**. Huduma za matibabu ndani na nje ya Zanzibar zitalipwa na Serikali.

**6**. Huduma za Maji na umeme zitalipwa na Serikali.

**7**. Watumishi wawili na mlinzi mmoja.

**8**. Posho la simu kwa kila mwezi kwa kiwango cha Shilingi laki tano.

**9**. Gari mbili zitakazotolewa na Serikali na kubadilishwa kila baada ya miaka mitano, na dereva wawili.

**10**. Posho la mafuta, matunzo na gharama za kuendeshea gari kama itakavyotolewa kwa Waziri katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kila gari.

**11**. Ulinzi wa nyumbani.

**12**. Hati za kusafiria zenye hadhi ya kidiplomasia na matumizi ya kumbi za watu mashuhuri kwa ajili yake, mwenza, baba, mama na watoto wake walio chini ya umri wa miaka kumi na nane.

**13**. Malipo ya gharama za safari daraja la kwanza ambayo yatahusisha mwenza wake na msaidizi binafsi mmoja wakati anapotakiwa kusafiri na Serikali au taasisi za kimataifa ndani na nje Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania au kwa ajili ya kusafiri kimatibabu ndani na nje ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania yatahusisha dereva.

**14**. Malipo ya gharama za safari binafsi daraja la kwanza ambayo yatahusisha mwenza na zisizozidi tatu kwa mwaka ndani ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo pia yatahusisha msaidizi binafsi, na safari hazitozidi siku kumi.

**D: MAELEZO YA MAFAO ANAYOPEWA NAIBU SPIKA MSTAAFU**

**1**. Kiinua mgongo sawa na asilimia maalumu ya mshahara wa mwisho aliowahi kupokea ukizidishwa na idadi ya miezi aliyoshika nafasi hiyo kama Naibu Spika.

**2**. Posho la hitimisho la kazi sawa na asilimia maalumu ya mshahara wa mwisho aliowahi kupokea ukizidishwa kwa miezi ishirini na nne ukizidishwa kwa idadi ya miaka aliyotumikia ikigaiwa kwa tano.

**3**. Hati ya kusafiria yenye hadhi ya kidiplomasia kwa ajili yake na mwenza wake.

**4**. Gari moja itakayotolewa na Serikali na kubadilishwa kila baada ya miaka mitano, na dereva mmoja.

## JADWELI LA PILI

## UTARATIBU WA UTOAJI WA MAFAO KWA MWANASHERIA MKUU MSTAAFU, WAZIRI MSTAAFU, NAIBU WAZIRI MSTAAFU NA MJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
**[Chini ya kifungu cha 19]**

---

**1.** Kiinua mgongo sawa na asilimia maalumu ya mshahara wa mwisho aliowahi kupokea ukizidishwa na idadi ya miezi aliyotumikia.

**2**. Posho la hitimisho la kazi sawa na asilimia maalumu ya mshahara wa mwisho aliowahi kupokea ukizidishwa kwa miezi ishirini na nne ukizidishwa kwa idadi ya miaka aliyotumikia ikigaiwa kwa tano.

**3**. Hati ya kusafiria yenye hadhi ya kidiplomasia kwa Waziri mstaafu, Naibu Waziri Mstaafu na Mwanasheria Mkuu Mstaafu, mwenza na watoto wake walio chini ya miaka kumi na nane.

## JADWELI LA TATU

## MAFAO KWA MWENZA, MJANE WA KIKE AU MJANE WA KIUME WA RAIS MSTAAFU, MAKAMO WA RAIS MSTAAFU NA WA SPIKA MSTAAFU

**[Chini ya kifungu cha 22]**

---

### A: MAELEZO YA MAFAO ANAYOPEWA MWENZA, MJANE WA KIKE AU MJANE WA KIUME WA RAIS MSTAAFU

**1**. Pencheni anayopewa mwenza wa Rais Mstaafu kwa mwezi sawa na asilimia themanini ya posho la mwezi analopewa mwenza wa Rais aliyopo madarakani.

2. Pencheni anayopewa mjane wa Rais Mstaafu kwa mwezi sawa na asilimia themanini ya mshahara wa mwezi anaopewa Rais aliyeko madarakani.

**3**. Gari moja itakayotolewa na Serikali ambayo itabadilishwa kila baada ya miaka mitano, na dereva mmoja.

**4**. Huduma za kimatibabu kwa mwenza, mjane wa kike au mjane wa kiume na watoto walio chini ya miaka kumi na nane ndani na nje ya Zanzibar.

**5**. Msaidizi binafsi mmoja.

**6**. Malipo ya gharama za safari daraja la kwanza ambayo yatahusisha gharama za msaidizi binafsi mmoja wakati atakapotakiwa kusafiri na Serikali au taasisi za kimataifa ndani na nje ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na ikitokea kusafiri kimatibabu yatahusisha daktari binafsi.

**7**. Malipo ya gharama za safari Daraja la kwanza kwa ajili ya safari binafsi zisizozidi tatu kwa mwaka ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo zitajumuisha gharama za msaidizi binafsi, na safari haitozidi siku saba.

**8**. Huduma ya makaazi kwa mjane wa kike au mjane wa kiume wa Rais Mstaafu kama itakavyoamuliwa na Serikali.

### B: MAELEZO YA MAFAO ANAYOPEWA MWENZA, MJANE WA KIKE AU MJANE WA KIUME WA MAKAMO WA RAIS MSTAAFU

**1**. Pencheni anayopewa Mwenza wa Makamo wa Rais Mstaafu kwa mwezi sawa na asilimia themanini ya posho la mwezi analopatiwa mwenza wa Makamo wa Rais aliyopo madarakani.

**2**. Pencheni anayopewa mjane wa Makamo wa Rais Mstaafu kwa mwezi sawa na asilimia themanini ya mshahara wa mwezi anaopatiwa Makamo wa Rais aliyeko madarakani.

**3**. Gari moja itakayotolewa na Serikali ambayo itabadilishwa kila baada ya miaka mitano, na dereva mmoja.

**4**. Huduma za kimatibabu zitatolewa na Serikali kwa ajili ya mwenza, mjane wa kike au mjane wa kiume na watoto walio chini ya miaka kumi na nane ndani na nje ya Zanzibar.

**5**. Msaidizi binafsi mmoja.

**6**. Malipo ya gharama za safari daraja la kwanza ambayo yatahusisha gharama za msaidizi binafsi mmoja wakati atakapotakiwa kusafiri na Serikali au taasisi za kimataifa ndani na nje ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na ikitokea kusafiri kimatibabu yatahusisha daktari binafsi.

**7**. Malipo ya gharama za safari Daraja la kwanza kwa ajili ya safari binafsi zisizozidi mbili kwa mwaka ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo yatahusisha msaidizi binafsi, na safari haitozidi siku tano.

**8**. Huduma ya makaazi kwa mjane wa kike au mjane wa kiume wa Makamo wa Rais Mstaafu kama itakavyoamuliwa na Serikali.

**C: MAELEZO YA MAFAO ANAYOPEWA MWENZA, MJANE WA KIKE AU MJANE WA KIUME WA SPIKA MSTAAFU**

**1**. Pencheni inayotolewa kila mwezi kwa mjane wa kike au mjane wa kiume wa Spika mstaafu sawa na asilimia arobaini ya mshahara wa mwezi anaopewa Spika aliyopo madarakani.

**2**. Huduma za matibabu kwa ajili ya mwenza, mjane wa kike au mjane wa kiume wa Spika mstaafu ndani na nje ya Zanzibar.

## MADHUMUNI NA SABABU

Madhumuni na sababu ya Mswada huu ni Kufuta Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu, Nam. 2 ya 2012, na Kutunga Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Kisiasa, 2025, kwa lengo la kuimarisha na kuweka utaratibu mzuri wa utowaji wa mafao na matunzo kwa Viongozi wanaostaafu utumishi wa kisiasa pamoja na wenza wao, kwa mujibu wa masharti ya Mswada huu.

Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu yanasimamiwa na Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu, Nam. 2 ya 2012, ambapo utekelezaji wa Sheria hiyo unakabiliwa na changamoto nyingi kutokana na kuwepo kwa baadhi ya stahiki ambazo haziendani na hali halisi ya maisha ya sasa ya Viongozi hao. Hivyo, Mswada unaopendekezwa umeimarisha baadhi ya stahiki hizo ili kuendana na hali halisi ya maisha ya sasa ya Viongozi hao pamoja na wenza, wajane wao wa kike na wa kiume.

Mswada unaopendekezwa wa kufuta Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa Wastaafu Nam. 2 ya 2012, na Kutunga Sheria ya Mafao ya Kustaafu Utumishi wa Kisiasa, 2025, umegawika katika sehemu 5:

***Sehemu ya Kwanza*** inahusu masharti ya awali ambayo yanajumuisha jina fupi na kuanza kutumika kwa Sheria pamoja na ufafanuzi wa maneno yaliyotumika katika Mswada.

***Sehemu ya Pili*** inaelezea kuhusu masharti yanayosimamia utoaji wa mafao, ikijumuisha mawanda ya kustahiki kupatiwa mafao, kutokua na sifa ya kustahiki mafao, upokeaji wa mafao ya kumaliza utumishi kutoka mifuko myengine na msamaha wa kodi ya mapato.

***Sehemu ya Tatu*** inaweka masharti kuhusu utoaji wa mafao kwa Rais Mstaafu, Makamo wa Rais Mstaafu, Spika Mstaafu na Naibu Spika Mstaafu.

***Sehemu ya Nne*** inaelezea kuhusu mafao yanayotolewa kwa Mwanasheria Mkuu Mstaafu, Waziri Mstaafu, Naibu Waziri Mstaafu na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi Mstaafu.

***Sehemu ya Tano*** inaelezea kuhusu masharti mengineyo ikiwemo kuzuiliwa kulipwa mafao, mafao kwa mwenza na mjane wa Rais Mstaafu, Makamo wa Rais Mstaafu na Spika Mstaafu, muda wa malipo ya kiinua mgongo na posho la hitimisho la kazi, ugawaji wa kiinua mgongo kwa wategemezi, uwezo wa kurekebisha Jadweli, uwezo wa Rais kutoa mafao ya ziada, kanuni, na kufuta na kubakiza.

**ZANZIBAR** ( MHE. ALI SULEIMAN AMEIR)
10 Febuari, 2025 **WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS IKULU ZANZIBAR**

**LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI - ZANZIBAR 2025**